

OFISI YA RAIS - TAMISEMI

HALMASHAURI YA (W) LUSHOTO

SHULE YA SEKONDARI NGWELO,

S.L.P 177,

LUSHOTO,

___/12/2020,

Kumb No MBSS/JI/01/2020

JINA LA MWANAFUNZI_____

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA
SEKONDARI MBWEI 2021**

1: UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza 2021 katika shule hii ya Sekondari Mbwei. Unapongwezwa sana kwa kuwa mionganoni mwa vijana wachache waliopata nafasi ya kujiunga na shule za sekondari za Serikali. Tunategemea utaliezi Taifa lako kwa kufanya vizuri katika masomo na kila shughuli shulenii na kutumia nafasi hii vizuri.

Mhula wa kwanza wa masomo unategemea kuanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shulenii kuanzi tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti shulenii ni tarehe 18/01/2021

2: MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

SARE ZA SHULE

A. WAVULANA

- i. Sare ya shule hii ni suruali mbili rangi ya kijani kitambaa namba moja zisizobana
- ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi
- iii. Soksi nyeusi jozi mbili na viatuu vyeusi vya kufunga na kamba
- iv. Sweta rangi ya blue bahari

B. WASICHANA

- i. Sketi mbili za rangi ya kijani kitambaa namba moja ndefu za heshima. Mshono rinda box
- ii. Mashati mawili ya rangi nyeupe na hijabu nyeupe zisizo na urembo kwa waislam
- iii. Soksi nyeupe jozi mbili na viatu vyeusi visigino vifupi vya kufunga na kamba
- iv. Sweta rangi ya blue bahari

3: VIFAA VYA KUJIFUNZIA

Mwanafunzi anatakiwa kuja na daftari kubwa kumi (Quire 3) daftari ndogo kwa ajili ya mazoezi ya kila siku, Set ya vifaa vya hisabati, Kalamu za wino za kutosha, Penseli, Rula ndefu na Dictionary moja

NB: Vifaa hivi vitakaguliwa siku ya kuripoti

4: SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Sheria na kanuni hizi ni muhimu na zieleweke kuwa ndiyo dira na usalama wa shule

a) SHERIA ZA NCHI

Kila mwanafunzi analazimika kufuata sheria zote za nchi. Ni wajibu kuheshimu bendera ya taifa picha za viongozi wa Taifa, wimbo wa Taifa, fedha ya Taifa na Nembo ya Taifa

b) MASOMO

Shughuli zote zilizopangwa katika ratiba ya shule ni muhimu. Kila mwanafunzi anapaswa kufuata ratiba ya shule kama ilivyopangwa. Mwanafunzi anapaswa kuwahi asubuhi shuleni na kubaki shuleni hadi mwisho wa shughuli za siku. Mwanafunzi ataondoka shuleni kwa ruhusa maalum

c) MAADILI

i. HESHIMA

Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu walimu, wafanyakazi wa shule, viranja, wananchi, na wanafunzi wenzao hapa shuleni na nje ya shule.

ii. USAFI

Usafi wa mwili na mavazi ni muhimu hapa shuleni. Pia aje na fagio, ndoo, fykeo/jembe kwa ajili ya usafi

iii. NI MWIKO KWA MWANAFUNZI

Kuvuta sigara/ bangi kutumia madawa ya kulevy/a/ kunywa pombe, kutembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe au majumba ya kufikia wageni, kutumia lugha mbaya na zakihuni kwa wanafunzi wenzako, walimu na watu wengine.

iv. UVAAJI WA SARE NI LAZIMA KWA WANAFUNZI WOTE

i. Masomo darasanui

ii. Wanafunzi wanapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule.

iii. Maandamano

iv. Wanafunzi wanapokwenda hospitali

v. Mikutano

vi. Mhadhala wa Shule

v. TUNZA MAJENGO SAMANI VITABU NA VIFAA VYOTE VYA SHULE VIZURI

d) MIKUTANO NA MAWASILIANO.

Mikutano na mawasiliano yoyote hapa shuleni lazima ijulikane rasmi kwa mkuu wa shule

e) LUGHA

Masomo yote kasoro Kiswahili na Dini ya kiislamu yatafundishwa kwa Kiswahili masomo mengine yote yatafundishwa kwa kingereza, Tunasisitiza lugha ya kingereza kuwa lugha rasmi ya mawasiliano shuleni

v. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

i. Wizi

ii. Uasherati, Ubakaji na Ushoga

iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevy/a

iv. Kupiga au kupigana

v. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

vi. Kudharau bendera ya taifa na picha za viongozi

vii. Kuwa mjamzito au kupata mimba

viii. Kuoa au kuolewa

ix. Kutoa mimba

x. Kuongoza, kuchochea au kuvuruga amani ya shule

xi. Kukataa adhabu kwa makusudi

xii. Kuwa na simu ya mkononi

**Vi. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA
MWANAFUNZI SHULENI**

- (a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali
- (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkata wa kutoshiriki katika mgomo
- (c) Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

7: TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO/ MAAGIZO NA

KUYATEKELEZA KIKAMILIFU

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

**EMMANUEL COSMA KAWISHE
MKUU WA SHULE.**

**GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

SHULE YA SEKONDARI NGWELO,

S.L.P 177,

LUSHOTO,

___/12/2020,

MEDICAL OFFICER

MR/ _____

Please examine the above named pupil that he/she is physical and mental fit/unfit for full time schooling course

(a) (i) eye sight _____

(ii) Limbs _____

(iii) Speech _____

(v) Venereal disease _____

(vi) Leprosy _____

(vii) Epilepsy _____

(b) Neuroses _____

(c) Other serious disease (**mention**)

Pregnant test _____

Other important test (if
any) _____

Station _____ Name _____ Signature _____

Designation _____